**HOTUBA YA MLEZI WA CHAMA CHA SKAUTI TANZANIA MHE. DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, ITAKAYOSOMWA KWA NIABA YAKE NA MHE. SAMIA SULUHU HASSAN, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA UFUNGUZI WA SHEREHE ZA MIAKA 100 YA USKAUTI TANZANIA TAREHE 26 JULAI, 2017 MJINI DODOMA**

**Mhe. Balozi Seif Ali Iddi (MB) Makamu wa Rais, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar;**

**Mhe. Alhaj Ali Hassan Mwinyi, Rais Mstaafu Awamu ya Pili;**

**Mhe. Benjamin William Mkapa, Rais Mstaafu Awamu ya Tatu;**

**Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais Mstaafu Awamu ya Nne;**

**Mhe. Dkt. Salim Ahmed Salim, Waziri Mkuu Mstaafu na Katibu Mkuu Mstaafu OAU;**

**Mhe. Philip Mangula, Makamu Mwenyekiti Chama cha Mapinduzi;**

**Mhe. Jordan Rugimbana, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma;**

**Mhe. Prof. Joyce Ndalichako (MB), Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi na Rais wa Chama cha Skauti Tanzania;**

**Muadhama Kardinali Polycap Pengo – Kiongozi Kanisa Katoliki Tanzania;**

**Sheikh Abubakari Zuberi - Mufti Mkuu Tanzania;**

**Prof. Philemon Sarungi - Makamu wa Rais wa Chama cha Skauti Tanzania na Mwenyekiti Jamii – Tanzania;**

**Mhe. Eng. Stella Manyanya, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi;**

**Dkt. Akwilapo - Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi;**

**Prof. Idris Kikula – Makamu Mkuuwa Chuo Kikuu Dodoma;**

**Mhe. Mwantumu Bakari Mahiza Skauti Mkuu wa Chama cha Skauti Tanzania;**

Scanned by CamScanner

**Mhe. Abdulkarim Esmail Hassan Shah Kamishna Mkuu wa Chama cha Skauti Tanzania;**

**Wahe. Mawaziri na Naibu Mawaziri;**

**Wahe. Wakuu wa Taasisi za Umma za Kupambana na Rushwa, Dawa za Kulevya, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Wakala wa Misitu;**

**Wahe. Wakuu wa Mikoa na Wilaya;**

**Wajumbe Kamati ya Ulinzi na Usalama Taifa na Mkoa;**

**Makamishna wa Skauti Mkoa na Wilaya;**

**Waandishi wa Habari;**

**Maskauti Wote Waliohudhuria Hadhara Hii;**

**Wageni Waalikwa;**

**Mabibi na Mabwana.**

**Habari za Mchana**

**Scout Motto!!................................**
**Scout we!!!!.................................**

Nianze kwa kuungana nanyi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema na Neema kwa kutujalia kuwepo hapa siku hii ya leo. Kwa wale wote mliofika Dodoma kwa mara ya kwanza naomba niwakaribishe Makao Makuu ya Nchi yetu.

## Salamu za Rais

Kwa namna ya kipekee naomba nimshukuru Mhe. Kasim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuelekeza sherehe hizi zifanyike Dodoma badala ya Arusha kama ilivyokuwa imepangwa awali.

Hii ni nafasi nzuri ya kuendelea kuutangaza Mkoa wa Dodoma ambao ndiyo Makao Makuu ya Nchi yetu, na ni fursa kwa vijana waliofika hapa kuyaona mandhari ya Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM). Naamini hali hii itawajengea vijana hawa ari na hamasa zaidi kwamba siku moja na wenyewe wawe ni sehemu ya Chuo hiki kikubwa kabisa katika nchi yetu.

Scanned by CamScanner

Kwa dhati niwapongeze Skauti Tanzania kwa kutimiza miaka 100. Hii ni hatua kubwa kwenu na jambo la kujivunia kwangu kama mlezi wenu. Naomba pia niwashukuru kwa risala yenu nzuri ambayo imenipa taswira mimi Mlezi wenu kujua yale yanayotendeka katika Chama hiki cha Skauti.

**Waheshimiwa Viongozi;**
**Ndugu Wana Skauti na Wananchi;**

Maadili ya Chama cha Skauti na Wanachama wake yanatokana na muundo wa Uongozi wa Chama uliopo. Ninawapongeza kwa dhati Viongozi wote wa Chama kwa kujenga na kulea maadili mema na kupambana na mmomonyoko wa maadili katika jamii yetu. Tangu kilipoasisiwa Chama kilijikita kwenye malezi na makuzi ya vijana, ujasiri, ukakamavu na uzalendo, kuwasaidia watu siku zote na kuzitii Sheria na Kanuni za nchi. Mambo haya kwa sasa yanahitaji kusisitizwa zaidi kuliko wakati mwingine wowote, kwa kuwa Taifa letu linakabiliwa na mmomomyoko wa maadili kwa Vijana wetu. ni vyema kwa Taasisi kama hizi (Scout na Girl Guides) zikakaza mwendo kwenye kutekeleza majukum yake.

Ingependeza kuona katika maisha ya kila siku hapa Tanzania, Vyama hivi vinabadilisha na kuwajengea Vijana wetu Wasichana na Wavulana, mwelekeo wa kujitambua, tabia njema na stadi za maisha zitakazowawezesha kujitoa katika kusaidia kujenga Jamii ambayo kila mmoja wetu angefurahia na kujivunia kuishi nayo. Mimi mlezi wenu nitajisikia vyema kufanyakazi nanyi katika kuwajenga Vijana wetu na Maarifa, kuwalea katika misingi ya kizalendo, kuwaelekeza kujiamini ili tujenge Taifa la Vijana wema inavyowezekana.

Kazi ya kutengeneza Vijana wenye sifa za Uzalendo, Uadilifu, Uaminifu na wanaoelewa jinsi ya kuishi na wengine ni jambo muhimu katika kuzalisha Viongozi wa baadae katika Jamii yetu. Ninachotaka kuwaeleza na muondoke nacho kutoka sherehe hizi ni kwamba Kijana wa Skaut au Girl Guide lazima ujengwe na utashi wa kurudisha fadhila kwa jamii yako. Ninyi mliopo hapa na wengine ambao hawakuweza kufika hapa leo, mlibahatika kulelewa, kufunzwa na kuelekezwa maadili mema, na mambo ya msingi yatakayowasaidia kuendesha maisha yenu (Life Skills). Mkiyatekeleza na kuyafuata mafundisho hayo yatakusaidieni kukutenganisheni na watu waovu. Mkijikusanya na kutumia ujuzi wenu mnaweza mkatoa msaada kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Kwa bahati nzuri Chama hiki kimesukwa na Wazee na Vijana wenye hekima na busara katika kulinda mila na desturi zetu njema. Naamini tukiamua tunaweza kabisa kuendelea kuwa na Taifa bora kabisa katika maadili na ustawi wa jamii yetu (Rushwa, Ufisadi, Usaliti Uzembe na Wizi).

**Ndugu Wana Skaut,**
Kwa mujibu wa Katiba ya Skaut, Rais wa Nchi ndie mlezi wa Chama hiki, kwa minajili hiyo, nitumie fursa hii maalum kuwashukuru na kuwapongeza Marais Wastaafu waliotangulia kuwa Walezi wa Skauti Tanzania kabla yangu. Kwa hakika wamelea Skauti katika nyakati za Raha na Changamoto, ila, wamelea kwa Utashi Mkubwa, kwa

Scanned by CamScanner

Uzalendo na Kujiamini na kwa Huruma. Ndugu Wahe. Marais Wastaafu, mmeweza kutekeleza Dhima (Mission) ya chama kwa uhodari mkubwa.

Mtakumbukwa daima kwa mapenzi na maelekezo yenu katika kuongoza Dira ya Chama hiki. Mcheza Kwao hutunzwa, inafurahisha kuona kwamba Skauti imetambua mchango mkubwa mlioutoa na leo hii kuamua kukupeni Tunzo zinazotunuku jitihada zenu.

Pamoja nanyi niwapongeze pia Rais wa Skaut Tanzania, Skauti Mkuu, Kamishna Mkuu na Makamishna wa Mikoa na Wilaya na Viongozi wote wa Skaut waliopo na waliostaafu, kwa kazi kubwa ya ulezi wa Vijana na kuendesha Chama hiki.

Skaut ni Chama kikongwe na chenye mtandao wa ndani na nje ya Nchi, hivyo kwa maadhimisho haya ya miaka 100 ni dhahiri kwamba, hiki sasa ni Chama kilichokomaa. Nafahamu kuwa wakati chama hiki kinaanzishwa mwaka 1917 kilikuwa na wanachama wapatao 850. Nimefahamishwa kuwa kwa sasa chama kina zaidi ya wanachama milioni nne. Ongezeko hili kwa miaka 100 bado halitoshi, tujitahidi wanachama wetu waongezeke zaidi ya hapo.

**Ndugu Wana Skaut,**
Nawashukuru kwa kunipongeza kwa utendaji wangu na kuwajibika kwa wananchi ambao ndio walionipatia ridhaa ya kuongoza nchi hii. Aidha, sina budi kuwatumikia wananchi kwa nguvu zangu zote tena bila kujali itikadi za vyama, dini zao, makabila yao, rangi zao n.k.

Naamini kila Kiongozi akijituma kwa faida ya nchi yetu tutapata maendeleo makubwa na ya haraka zaidi.

**Waheshiwa Viongozi,**
**Ndugu Wana Skauti na Wananchi,**

Historia ya Chama cha Skauti imeanza mwaka 1917 kabla ya uhuru wa Tanganyika. Mtu aliyezaliwa mwaka huo hadi tunapata uhuru mwaka 1961 alikuwa na miaka 44. Inawezekana kabisa wapo waliopitia Uskauti na walitoa mchango mkubwa katika kupatikana kwa Uhuru wa Nchi yetu. Mmewataja baadhi ya mashujaa wakiongozwa na Baba wa Taifa ***Hayati Mwl. Julius Kambarage Nyerere*** ambaye ndiye alikuwa Mlezi wa Chama hiki wa Kwanza. Jambo zuri mnaloweza kuwaenzi Mashujaa hao ni kwa kuchapa kazi kwa bidii kubwa kwani Wahenga wetu hao walituambia **"UHURU NI KAZI"** na **"KAZI NDIO KIPIMO CHA UTU"**, kwa kutafakari na kutafsiri hayo ndio serikali yenu ikaja na wito wa **"HAPA NI KAZI TU"**.

Hata hivyo, kufikia miaka 100 ni safari ndefu iliyopita milima na mabonde na kukabiliana na changamoto nyingi, kama tujuavyo, maisha hayana tambarare wala mteremko. Hata hivyo, kukabiliana na milima kunatupatia uzoefu wa safari yenyewe. Hivyo naamini mnao uzoefu wa kutosha katika tasnia na taaluma za Kiskauti.

Scanned by CamScanner

Hivyo basi, uzoefu na uwezo mliojijengea muutumie vyema katika kuzifanyia kazi changamoto zinazowakabili ili kuzigeuza kuwa fursa. Matarajio yangu ni kwamba mkiwa wabunifu na kwa kushirikiana na asasi mbalimbali, changamoto mlizozitaja zitakuwa historia kwa siku za usoni.

**Ndugu Wana Skaut,**
Kwa kusaidia tu mawazo, baadhi ya changamoto zilizobainishwa, zinatatulika kwa kufanya mambo yafuatayo:-

1. Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ziangalie uwezekano wa kuwapatia Ofisi ili kazi zenu zifanyike kwa ufanisi.

2. Maafisa Ardhi Mikoa na Wilaya watenge maeneo kwa ajili ya shughuli za uzalishaji na kambi za vijana skauti, kama ni mashamba, mifugo n.k navyo viwe darasa kwa wanaozunguka maeneo hayo.

3. Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya ambao nao ni walezi kwa niaba yangu, wawasaidie vijana wa skauti kutekeleza shughuli zao zenye manufaa kwa Taifa.

4. Wakuu wa Vyuo, Wakuu wa Shule za Sekondari na Shule za Msingi, Taasisi za Dini, zingatieni Waraka wa Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi kuhusu kazi za ziada. Wakaguzi wa Elimu wataendelea kukagua jinsi vituo vyenu vinavyoendesha shughuli nyingine za kuwajenga vijana nje ya masomo, yaani ***"Extra curriculum activities".***

Aidha, anzisheni miradi ambayo itawashirikisha vijana na toeni mafunzo ya stadi mbalimbali za kazi ili ziwawezeshe vijana wa marika yote kuweza kujiajiri ili kukabiliana na ukosefu wa ajira.

Binafsi nimefurahishwa sana na miradi ambayo Chama kimeshirikiana na Wananchi katika kuitekeleza na hatimaye kujiletea maendeleo. Jitihada hizi ziendelee. Niwatake Viongozi wa Serikali kuunga mkono jitihada hizi pale watakapohitajika kufanya hivyo, mtakuwa mnafanya kwa ajili ya Watanzania na Taifa la Tanzania.

Sambamba na hayo, ninawataka kuheshimu kiapo chenu na kwamba msijiingize kwenye mambo ambayo yataharibu weledi wenu. Kuweni watii kwa Mungu na kwa Taifa lenu, wasaidieni watu siku zote na kuzitii Kanuni za Skauti.

**Ndugu Wazazi,**
Naomba nitoe wito kwenu kuwaruhusu vijana wenu kujiunga na kundi zuri la Chama cha Skauti Tanzania.

Scanned by CamScanner

**Waheshimiwa Viongozi,**
**Ndugu Wananchi,**

Katika kumalizia hotuba yangu, Niwashukuru na kuupongeza Uongozi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kwa kuwa wenyeji wetu, Takukuru, Mamlaka ya Udhibiti Madawa ya Kulevya, TACAIDS, Usalama Barabarani, Sekretarieti ya Tume ya Maadili ya Viongozi, Chakula na Lishe, Jeshi la Uokoaji na Zimamoto kwa kutenga muda wenu na kuja kutoa Mafunzo kwa Skauti ili na wao waweze kufikisha elimu hiyo kwa jamii na hata Mashuleni na Vyuoni.

Aidha, ninawapongeza Kamati Kuu ya Maandalizi pamoja na wote walioshiriki na kusaidia kufanikisha maadhimisho haya. Nakushukuruni nyote na kuwatakia kila la kheri katika kuendeleza Uskauti na Ujenzi wa Taifa letu.

Mwisho, natamka kwamba Maadhimisho haya ya miaka 100 ya Chama cha Skauti Tanzania yamefunguliwa rasmi na kwamba niko tayari kupokea Tuzo mliyoniandalia.

**Asanteni kwa kunisikiliza.**

Scanned by CamScanner